


**HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA
SHULE YA SEKONDARI MWAYA**



**S.L.P 215
MAHENGE/ULANGA**

Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE

Ninayofuraha kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na shule ya **Sekondari Mwaya** kidato cha kwanza mwaka wa masomo 2021 baada ya kufaulu mtihani wa darasa la saba. Uongozi wa shule unampongeza na kumkaribisha **Mwaya Sekondari**.

Shule ya Sekondari Mwaya ni shule ya kutwa kwa wavulana na wasichana.

Shule itafunguliwa rasmi muhula wa kwanza tarehe **11/01/2021** saa 01:00 asubuhi.

mfikapo shuleni ripoti ofisi ya makamu mkuu wa shule kwaajili ya usajili.

Kauli mbiu ya shule ni: **ELIMU NI HAZINA (EDUCATION IS TREASURE)**

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. SARE YA SHULE

a) Wavulana

- ✚ Suruali mbili nyeusi (mshono wa kawaida sio jinsi staili wala isiwe modo) akiwa na modo au jinsi staili hatapokelewa
- ✚ Shati mbili nyeupe mikono mifupi
- ✚ Sweta moja rangi ya blue/bendera ya taifa
- ✚ Viatu vyeusi vya ngozi kisigino kifupi vya kamba
- ✚ Soksi rangi nyeupe
- ✚ Mkanda mweusi
- ✚ Tai nyeusi

b) Wasichana

- ✚ Sketi mbili nyeusi (kitambaa kizito) ndefu kupita magoti (mshono rinda box) akija na sketi fupi hatapokelewa
- ✚ Kwa waislamu Hijab rangi nyeupe tu.
- ✚ Shati mbili nyeupe
- ✚ Sweta moja rangi ya blue/bendera ya taifa
- ✚ Viatu vya ngozi vya kufunika kisigino kifupi (vya kamba)
- ✚ Soksi rangi nyeupe
- ✚ Tai nyeusi
- ✚ Tshirt ya shule

VIFAA VYA DARASANI

- Daftari kubwa kumi na mbili (Caunter book)
- Peni, penseli, ufutio, mkebe na begi la kubebea daftari.

VAFAA VYA MICHEZO (Lazima)

- ❖ Raba jozi moja
- ❖ Track na tshirt yake (rangi jezi ya Mbeya city ambayo ni zambarau)

SHERIA ZA SHULE

A: HESHIMA

- i. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri apitapo, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano
- ii. Mwanafunzi haruusiwe kutumia lugha mbaya wakati wowote kati yao wenyewe, kwa walimu wao au kwa watu wengine
- iii. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote waliopo shuleni
- iv. Mwanafunzi anapaswa kushirikiana na kusaidia katika kazi
- v. Mwanafunzi anapaswa kuthamini kazi za aina zote shuleni
- vi. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mambo yafuatayo:
 - a) Kuvuta sigara
 - b) Kufuga kucha, ndevu na nywele
 - c) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima
 - d) Kugombana
- vii. Mwanafunzi anatakiwa kuitika mara moja na kukimbilia aliko mkuu aliyemuita
- viii. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa serikali, nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na fedha za Taifa
- ix. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu ofisi za shule, mali ya binafsi na mali ya umma.
- x. Mwanafunzi anatakiwa kusimama katika mstari wakati wa kupokea huduma
- xi. Mwanafunzi anatakiwa kukaa kiny wakati wote akiwa darasani, asitoke nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko.

B: MAHUDHURIO

- i. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria shule kwa muda wote wa masomo
- ii. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa


- iii. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria katika kazi zote za mikono
- iv. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa.

C: MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

- i. Wizi wa aina yoyote
- ii. Uasherati, ubakaji na ushoga
- iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
- iv. Uvutaji bangi
- v. Utoro wa siku 90 mfululizo
- vi. Kutokufanya mitihani na majaribio
- vii. Kukutwa na simu na matumizi ya simu katika mazingira ya shule
- viii. Kupigana au kupiga
- ix. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- x. Kudharau bendera ya Taifa
- xi. Kutembelea sehemu za starehe kama bar, guest na vibanda vya video
- xii. Kuo au kuolewa
- xiii. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
- xiv. Kutoa mimba
- xv. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu
- xvi. Kukataa adhabu kwa makusudi

Hivyo anatakiwa kuzingatia sheria za shule ili aweze kuendelea kuwa mwanafunzi wa Mwaya Sekondari.

**NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA
"ELIMU NI HAZINA DUNIANI"**



FADHILI GOLDEN KIMANGA, IER

Mkuu wa Shule

**THE HEADMASTER
MWAYA SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 215
MAHENGE H/MF/**